

## **MAENDELEO YA JAMII**

### **UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA KIUCHUMI VYA WANAWAKE NA VIJANA**

Manispaa ya **Mtwara-Mikindani** imeendelea kuzingatia agizo la serikali la kuwezesha vikundi vya kiuchumi vya wanawake na vijana kwa kutenga **(10%)** ya mapato yake ya ndani na kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa vikundi hivyo.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilitoa mkopo wa jumla ya **Tsh.313,200,000.00**(Milioni mia tatu kumi na tatu na laki mbili elfu tu.) kwa vikundi 105 vikiwemo vikundi vya vijana 23 na wanawake 82. Jumla ya wanavikundi 1294 walinufaika na mkopo huo kati yao wanawake **1040** na vijana **254**.

Kwa mwaka huu wa fedha **2017/2018** Halmashauri inatarajia kutoa mikopo yenye thamani ya **Tsh 487,514,286.00** ikiwa ni asilimia 10% ya mapato yake ya ndani kwa vikundi **110**.

Aidha Halmashauri imechangia kwenye mfuko **TZS 165,000,000** sawa na asilimia **94%** kati ya **TZS 175,025,252.02** zilizotakiwa kuchangiwa kwenye mfuko hadi **Nov 2017**. Mikopo yenye thamani ya Tsh **152,680,000.00 (Milioni mia moja hamsini na mbili laki sita na elfu themanini )** imetolewa kwa vikundi **48** vikiwemo vikundi vya vijana **8** na vya wanawake **40** vyenye jumla ya wanufaika **240** ambapo kati yao wanawake ni **200** na vijana ni **40**. Mchanganuo wa mwenendo wa uchangiaji na utoaji wa mikopo kwa vikundi katika Halmashauri ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na 12

**Jedwali Na 13: Mwenendo wa utoaji wa mikopo kuanzia 2015/16 hadi 2017/2018**

| Mwaka          | Mkopo          | Mkopo na riba  | Idadi ya vikundi | Vijana | Wanawake | Marejesho      | %     | Baki ya deni   | Maelezo  |
|----------------|----------------|----------------|------------------|--------|----------|----------------|-------|----------------|--|
| <b>2015/16</b> | 140,000,000.00 | 154,000,000.00 | 86               | 13     | 76       | 141,382,000.00 | 93.8% | 9,694,500      | Hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa wadaiwa wote |
| <b>2016/17</b> |                |                |                  |        |          |                |       |                |  |
| Desemba        | 35,000,000.00  | 38,500,000.00  | 17               | 5      | 12       | 18,740,500.00  | 53%   | 17,919,500     | Ufuatiliaji unaendelea.                                    |
| Machi          | 91,700,000.00  | 100,870,000.00 | 27               | 5      | 22       | 38,616,000.00  | 38%   | 62,254,000.00  | Marejesho yameanza mwezi Mei .                             |
| Mei            | 125,000,000.00 | 137,500,000.00 | 40               | 10     | 30       | 38,727,000.00  | 28%   | 100,453,000.00 | Marejesho yameanza mwezi Julai 2017.                       |

|                  |                |                |     |    |     |                |    |                |  |
|------------------|----------------|----------------|-----|----|-----|----------------|----|----------------|--|
| Septemba         | 61,500,000.00  | 67,650,000.00  | 21  | 4  | 17  | 6,330,000      | 9% | 61,320,000.00  | Marejesho yameanza mwezi Desemba 2017. |
| <b>2017/2018</b> | 152,680,000.00 | 167,948,000    | 47  | 8  | 39  | -              | -  | 167,948,000    | Marejesho yataanza March 2018          |
| <b>JUMLA</b>     | 605,880,000.00 | 666,468,000.00 | 467 | 82 | 391 | 243,795,500.00 |    | 419,589,000.00 |  |

